



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA



Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, SLP 113, Iselamagazi,  
SHINYANGA Simu/Fax: 0282-986382 Barua pepe: [info@shinyangadc.go.tz](mailto:info@shinyangadc.go.tz)

Website: [www.shinyangadc.go.tz](http://www.shinyangadc.go.tz)

**Unapojibu tafadhali taja:**

*Kumb.Na.SDC/ C.4/7/Vol.I/49*

13.08.2021

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kupitia Kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/376/01"B"/60 cha tarehe 19 Julai, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (UTUMISHI) anatangaza nafasi ya kazi kwa Wananchi wa Tanzania wenye şifa na ujuzi wa kujaza nafasi ifuatayo:-

### I: Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (Nafasi 1)

#### (a) Sifa za Mwombaji:

- Awe amehitimu Kidato cha Nne au Sita na Cheti cha Mafunzo (NTA LEVEL 5) katika fani mojawapo kati ya hizi; - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology). Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### (b) Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja III

Mtendaji wa Kijiji atatekeleza majukumu yafuatayo.-

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao,
- Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji,
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mikutano Mikuu na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji,
- kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika ngazi ya Kijiji.

#### (c) Ngazi ya Mshahara:

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya TGS B kwa mwezi.

